

**Wayne N. Walters, Ed.D. Msimamizi wa Shule**

341 S. Bellefield Avenue  
Pittsburgh, PA 15213

[superintendentwalters@pghschools.org](mailto:superintendentwalters@pghschools.org)  
412-529-3600

[www.pghschools.org](http://www.pghschools.org)

Nambari ya Dharura ya Mzazi: 412-529-  
HFI P (4357)

Desemba 21, 2022

Wapendwa Wazazi/Walezi/Watoa Maamuzi wa Kielimu:

Natumai wote mko salama tunapoendelea kufanya tuwezavyo kujielekeza na kujirejesha katika kipindi hiki. Zaidi ya hayo, ninakushukuru kwa kuendelea kujitolea kwa Shule za Umma za Pittsburgh kama Mshikadau Muhimu.

Shule za Umma za Pittsburgh zinatambua elimu kukatizwa kwa ajili ya a janga hili na athari kwa wanafunzi wote na taifa letu. Kutokana na elimu kukatizwa, wanafunzi walemavu (Mipango ya IEPs na 504) wanaweza kuwa wanafaa kupata Huduma za Fidia ya Covid ikiwa hawakupokea tathmini au huduma ambazo walistahili kupata kuanzia Machi 16, 2020, hadi Juni 16, 2022 (Kipindi cha Janga).

Kama mzazi/mlezi/mtoa maamuzi ya kielimu wa mtoto aliye na mpango wa IEP au 504, ninakufahamisha mimi binafsi kwamba Shule za Umma za Pittsburgh zina mpango mpya wa Huduma za Fidia ya Covid, unaoitwa CCS 2.0, za kushughulikia athari za janga hili kwa wanafunzi wetu walemavu.

Wilaya itafanya mikutano ya IEP na 504 kwa wanafunzi wote wanaostahiki ili kubaini hasara yoyote ya elimu kutokana na Kipindi cha Janga na aina na kiasi cha Huduma za Fidia ya Covid itakayotolewa kwa mwanafunzi ili kushughulikia hasara iliyotambuliwa.

Hatua ya kwanza katika mpango huu ni kwa Timu ya Mpango wa IEP au 504 ya mtoto wako kukutana ili kubaini kiwango ambacho mtoto wako anafaa kupata Huduma za Fidia ya Covid kwa ajili ya huduma ambazo hazijatolewa au kupokewa wakati wa mafunzo ya mtandaoni, mafunzo mseto, ukatizaji unaoendelea unaohusiana na Covid wakati mafunzo ya ana kwa ana kurudi katika Kipindi cha Janga.

Iliyoambatishwa ni orodha ya ukaguzi ya kukusaidia kufikiria kuhusu elimu ya mtoto wako wakati wa Kipindi cha Janga na kujiandaa kwa ajili ya mkutano wa IEP/504. Kuingia mwaka wa 2023, utapokea sasisho na hatua zinazofuata kutoka kwa shule ya mtoto wako. Kwa maelezo zaidi kuhusu CCS 2.0, tafadhali tembelea [www.pghschools.org/CCS2.0](http://www.pghschools.org/CCS2.0). Tuko katika mchakato wa kuunda mifumo ya habari na viungo kwenye ukurasa wetu wa wavuti ili kukupa maelezo ya ziada.

Nakutakia wewe na familia yako kila la kheri tunapoelekea msimu ujao wa likizo.

Wako katika elimu,



Wayne N. Walters, Ed.D.  
Msimamizi wa Shule